SHERIA YA KUZUIA USAFIRISHAJI HARAMU WA BINADAMU

(SHERIA KUU)

MPANGILIO WA VIFUNGU

Kifungu *Jina*

SEHEMU YA I
MASHARTI YA AWALI

1. Jina kifupi na Uanzaji.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA II
ZUIO LA USAFIRISHAJI HARAMU WA BINADAMU

4. Vitendo vya usafirishaji haramu wa binadamu.
5. Vitendo vinavyoongeza au kufanikisha usafirishaji haramu wa binadamu.
6. Usafirishaji haramu wa binadamu wa hali ya juu.
7. Usafirishaji haramu wa binadamu kwa kutumia watu wa kati (Madalali).
8. Kuwatumia watu waliosafirishwa kiharamu.

SEHEMU YA III
UPELELEZI NA MWENENDO WA KIMAHAKAMA

9. Usiri.
10. Kutoa taarifa ya makosa.
11. Kuhojiwa na afisa polisi.
12. Kukamatwa na afisa wa polisi.
13. Kutenda kosa la pili na kuendelea.
14. Kutwaa na kutaifishwa kwa matunda na vifaa vilivyotokana na usafirishaji haramu wa binadamu
15. Fidia.
16. Utambuzi wa wahanga.

SEHEMU YA IV
UOKOAJI, MAREKEBISHO NA MSAADA KWA WAHANGA

17. Kuwaokoa, kuwajali, kuwawezesha kuishi maisha ya kawaida na kuwashauri watu waliosafirishwa kiharamu.
18. Ulinzi na msaada kwa wahanga.
19. Msaada na ulinzi kwa watoto wahanga.
20. Vituo kwa ajili ya ulinzi wa wahanga.

21. Kuwarudisha makwao wahanga.
22. Kuwarudisha makwao wahanga watoto au watu wenye ulemavu.
23. Kuwarudisha makwao raia wa nje, nk.
24. Programu zinazohusu usafirishaji haramu wa binadamu.

SEHEMU YA V
MFUKO WA KUKOMESHA USAFIRISHAJI HARAMU WA BINADAMU

25. Uanzishwaji wa mfuko wa kuzuia usafirishaji haramu wa binadamu.
26. Vyanzo vya mfuko.
27. Matumizi wa mfuko.
28. Usimamizi wa mfuko.
29. Fedha, akaunti na makisio ya mwaka ya sekretariati.

SEHEMU YA VI
KAMATI YA KUZUIA USAFIRISHAJI HARAMU WA BINADAMU

30. Uanzishwaji wa Kamati ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu.
31. Muundo wa Kamati ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu.
32. Kazi ya Kamati ya Kuzuia Usafirishaji haramu wa Binadamu.
33. Vikao vya kamati ya Kuzuia usafirishaji haramu wa Binadamu.

SEHEMU YA VII
MASHARTI MADOGO MADOGO

34. Ulinzi wa kisheria kwa watu waliosafirishwa kiharamu.
35. Fidia kwa wajumbe.
36. Matumizi ya sheria nyingine.
37. Kanuni.

SEHEMU YA VIII
MAREKEBISHO YATOKANAYO

38. Kufutwa kwa kifungu cha 139A.
39. Kurekebishwa kwa kifungu cha 148.
40. Kurekebishwa kwa kifungu cha 10.
41. Kurekebishwa kwa kifungu cha 3.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

SHERIA YA KUZUIA USAFIRISHAJI HARAMU WA BINADAMU

UTANGULIZI

KWAMBA Jamhuri ya Muungano inathamini utu wa kila binadamu na inahakikisha heshima kwa kila haki ya mtu;

NA KWAMBA Jamhuri ya Muungano inatambua haki sawa na utu wa asili wa watu kama ulivyowekwa kwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na kwenye Mkataba wa Kimataifa wa Kupambana na Uhalifu wa Kimataifa na Itifaki ya Kuzuia, Kuangamiza na Kuadhibu usafirishaji haramu wa binadamu na watoto na mikataba mingine ya haki za binadamu iliyokubaliwa, na mikataba ya kimataifa ambayo Tanzania ni mwanachama.

NA KWAMBA Jamhuri ya Muungano inatoa kipaumbele cha hali ya juu katika kuandaa mikakati na miradi ambayo inachochoea utu wa binadamu, inalinda watu kutokana na hatari ya ukatili na unyonyaji, inaondoa usafirishaji haramu wa binadamu na inapunguza vyanzo vya uhamiaji na kazi za kulazimishwa ka lengo la kuhakikisha wanaokolewa, Wanatibiwa na wanarudishwa kwenye mfumo wa jamii

NA KWAMBA Jamhuri ya Muungano inaamini kuwa licha ya kuwepo kwa mikataba mbalimbali ya kimataifa yenye kanuni na hatua za kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu, kuna umuhimu kuwa na sheria mahususi ili kutatua mambo yote yanayohusiana na usafirishaji haramu wa binadamu;

KWA HIYO INATUNGWA na Bunge la Jamhuri ya Muungano kama ifuatavyo:

SEHEMU YA I

MASHARTI YA AWALI

Jina kwa kifupi na Uanzaji	**1.-** (1) Sheria hii inaweza kuitwa Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, 2008. (2) Sheria hii itaanza kutumika katika tarehe ambayo Waziri anaweza kupanga, kwa taarifa itakayochapishwa kwenye Gazeti.
Matumizi	**2.**-(1) Sheria hii itatumika kwa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.
Tafsiri Sura ya 16	**3.** Katika hii Sheria isipokuwa kama maana itahitaji vinginevyo – ”utekaji” kuhusiana na makosa yanayohusiana na usafirishaji haramu wa binadamu maana yake ni kumlazimisha au kumshawishi mtu kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine; "afisa aliyeruhusiwa" maana yake ni afisa wa uhamiaji, afisa wa polisi au afisa mwingine wa umma anayetekeleza mamlaka ya sheria za mamlaka za utekelezaji; "msaada wa mambo ya msingi" inajumuisha elimu, afya, mavazi, malazi, ushauri na mahitaji wa mlo kamili; kulipwa na mtumiaji wa watu waliosafirishwa; "kuwekwa kwa dhamana" maana yake ni kuwekwa na msafirishaji kwa watu kwa nia ya kuwanyonya kwa ahadi ya msafirishaji "utunzaji na ulinzi" itakuwa na maana sawa na msaada ya mambo ya msingi; "mtoto" maana yake ni mtu aliye chini ya umri wa miaka kumi na nane; “deni" maana yake ni mdeni kutoa huduma yake mwenyewe au kazi au watu walio chini yake kama dhamana ay malipo ya deni, kama urefu wa kipindi na asili ya huduma hiyo havijawekwa bayana au

	thamani ya huduma kama ambavyo inatathiminiwa hailengi kumaliza deni husika; "mtu mwenye ulemavu" maana yake ni mtu ambaye hawezi kujihudumia, au kujilinda yeye mwenyewe dhidi ya dhuluma, utelekezwaji, ukatili, unyonyaji au ubaguzi kutokana na ulemavu wa viungo au akili; "unyonyaji" kuhusiana na usafirishaji haramu wa binadamu maana yake ni watu magendo ya watu, ukahaba na aina nyingine za unyonyaji wa kingono, kazi za kulazimishwa au huduma, utumwa au vitendo vinavyofanana na utumwa au kuondoa viungo vya mwili; "ajira ya kulazimishwa na utumwa" maana yake ni kufanyishwa kazi au kulazimishwa kutoa huduma kwa njia ya kushawishiwa, kupigwa, kutishwa, kutumia nguvu au lazima, ikijumuisha kumuondolea mtu uhuru, kumuondolea utu, dhamana ya deni au kudanganywa au kulaghaiwa; "mamlaka ya nje" maana yake ni mtu aliyekwa na serikali ya nje kama chombo chenye mamlaka ya kutenda kwa niaba ya serikali ya nje kwa madhumuni ya sheria hii; "Serikali" maana yake ni mamlaka ambayo utawala wa Jamhuri ya Muungano unatekelezwa; "majeraha" inajumuisha ya maumivu kimwili, kiakili na kisaikolojia; "Waziri" maana yake Waziri anayehusika na mambo ya ndani; "NGO" itakuwa na maana kama ilivyopewa chini ya Sheria ya Taasisi Zisizo za Kiserikali; "viungo" inajumuisha sehemu yoyote ya mwili wa binadamu ambayo inaweza kuondolewa ili kuendeleza maisha ya binadamu au kwa lengo linguine; "sehemu ya usalama" maana yake ni mahali

	ambapo usalama wa mhanga wa usafirishwaji unapatikana; "kuwekwa kama huduma" maana yake ni kuwekwa kwa mtu na msafirishaji kwa lengo la kunyonywa ambapo huduma ya mtu huyo hailipwi; "afisa wa polisi" inajumuisha afisa kutoka jeshi lolote lingine; "picha za ngono" inajumuisha mawasilisho yoyote, kupitia machapisho, maonyesho ya wazi, sinema, maonyesho ya utupu, teknohama au kwa njia yoyote nyingine, ya mtu anayehusika moja kwa moja au kwa kuwezeshwa katika shughuli za ngono au maonyesho ya aina yoyote ya viungo vya ngono kwa nia ya msingi ya kingono. "ukahaba" maana yake ni kitendo, mradi au mpango unaohusisha inayohusisha matumizi ya mtu na mtu mwingine kwa tendo la ngono au kitendo cha uasherati kwa kubadilishana na fedha, faida au kitu chochote cha thamani; "vyombo vya usalama" inajumuisha, Polisi, Mamlaka ya Mapato ya Tanzania, Uhamiaji na Idara ya Usalama wa Taifa; "afisa ustawi wa jamii" inajumuisha afisa ambaye hajathibitishwa kazini; "makazi ya muda" maana yake ni usafirishaji wa watu waliosafirishwa kiharamu kwa muda mfupi kwa ajili ya malengo ya kinyonyaji; "utalii wa ngono" maana yake- (a) programu iliyoandaliwa na kampuni au mtu anayehusika na usafiri au utalii, ambayo katika shughuli zake za kitalii, inatumia shughuli za ngono kama kivutio cha utalii; (b) huduma ya ngono au vitendo vinavyotolewa wakati wa kupumuzika au wakati wa mapumziko au burudani kwa wanajeshi; "unyonyaji wa kingono" maana yake uhusikaji wa mtu kwenye ukahaba au utengenezaji wa picha za ngono baada ya kutishiwa,

	kudanganywa, kulazimishwa, kutekwa, kutumia nguvu, matumizi mabaya ya madarak, dhamana ya madaraka, uongo au kwa kutumia udhaifu wa wahanga.
SEHEMU YA II KUZUIA USAFIRISHAJI HARAMU WA BINADAMU	
Vitendo vya usafirishaji haramu wa binadamu	**4.**-(1) Mtu anafanya kosa la usafirishaji haramu wa binadamu kama mtu huyo- (a) anaajiri, anasafirisha, anahamisha, anatunza, anatoa au kupokea mtu kwa njia yoyote, ikijumisha zile zinazofanyika kwa mgongo wa ajira za majumbani za nje ya nchi, mafunzo, ukahaba, picha za ngono, unyonyaji wa kingono, kazi za kulazimishwa, utumwa au dhamana ya deni; (b) anamtambulisha au anamuunganisha mtu na raia wa nje kwa njia ya ndoa kwa nia ya kumpata, kumnunua, kumtoa, kumuuza au kumfanya biashara mtu huyo ili mtu huyo aingizwe kwenye ukahaba, picha za ngono, unyonyaji wa kingono, kazi za kulazimishwa, utumwa au dhamana ya deni; (c) anaonyesha nia au anafunga ndoa, ya kweli au bandia, kwa nia ya kumpata, kummnunua, kumtoa, kumuuza au kumfanya biashara mtu huyo ili mtu huyo ahusishwe kwenye ukahaba, picha za ngono, unyonyaji wa kingono, kazi za kulazimishwa, utumwa, au dhamana ya deni; (d) kufanya au kuandaa utalii wa ngono au unyanyasaji wa kingono; (e) kumiliki au kukodi mtu kujihusisha na ukahaba au picha za ngono; (f) kuasili au kufanikisha kuasili mtu kwa nia ya ukahaba, picha za ngono, unyonyaji wa kingono, ajira ya kulazimishwa na utumwa na ya deni; (g) kuajiri, kukodi, kuasili, kusafirisha au kuteka- (i) mtu, kwa njia ya kutishia, au kwa kutumia nguvu, uongo, ulaghai,

	fujo, kulazimisha au kutishia kuondoa au kuuza kiungo cha mtu; au (ii) mtoto au mtu mlemavu kwa lengo la kumuingiza mtoto au mtu mlemavu kwenye shughuli za kijeshi. (2) Usafirishaji haramu wa binadamu utakuwa pia umetendeka kwa kuwekwa kwenye makazi ya muda au kazi kama nia yake ni kunyonywa na mtu mwingine. (3) Kama mhanga wa usafirishaji haramu wa binadamu ni mtoto, ridhaa ya mtoto, mzazi au mlezi haitakuwa kinga katika uendeshaji mashataka chini ya Sheria hii hata kama kuna ushahidi wa matumizi mabaya ya madaraka vibaya, ulaghai, uongo, kugandanya au udhaifu wa mtoto ulitumika kama sababu. (4) Ridhaa ya mhanga wa usafirishaji haramu wa binadamu haitakuwa kuwa na maana ikiwa kama njia zilizotajwa kwenye kifungu kidogo cha (1) zilitumika dhidi ya mhanga. (5) Mtu anayefanya kosa au kitendo kilichotajwa chini ya kifungu hiki atawajibika, kama akitiwa hatiani, kulipa faini isiyopungua shilingi milioni tano na isiyozidi shilingi milioni mia tano au kufungwa kifungo kisichopungua miaka miwili lakini kisichozidi miaka kumi au vyote.
Vitendo vinavyoongeza au kufanikisha usafirishaji haramu wa binadamu.	**5**.-(1) Mtu anayechochea au anayefanya au anayefanikisha utendekaji wa usafirishaji haramu wa binadamu anafanya kosa. (2) Mtu anachochea, anafanya au anafanikisha utendekaji wa usafirishaji haramu wa binadamu kama mtu huyo- a) kwa kujua anakodisha, anatumia au anaruhusu kutumika nyumba yoyote, jengo au makazi yoyote kwa lengo la usafirishaji haramu wa binadamu; b) anatengeneza, anachapa, anatoa au anagawa vyeti,

	usajili au kibandiko ambazo hazijatolewa, zimeghushiwa au ni za bandia za wakala yoyote wa serikali anayetoa vyeti, usajili au kibandiko kama uthibitisho kwa kuendana na matakwa ya serikali katika kuchocheausafirishaji wa binadamu ; c) anatangaza, anachapa au anagawa, au anafanikisha kutangazwa, kuchapwa au kugawiwa kwa njia yoyote, ikiwa ni pamoja na matumizi ya teknohama au kipeperushi, majarida au vyombo vingine ambavyo vinachochea usafirishaji haramu wa binadamu; d) anasaidia katika vitendo vya udanganyifu au ulaghai kwa nia ya kufanya au kufanikisha upatikanaji wa vibali na nyaraka nyingine muhimu kwaajili ya kwenda za kutoka nje ya nchi kutoka kwa wakala wa serikali kwa lengo la usafirishaji haramu wa binadamu; e) anafanikisha au anasaidia katika kutoka au kuingia katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mtu ambaye anamiliki nyaraka za kusafiria ambazo hazijatolewa, zimeghushiwa au ni za uongo kwa lengo la usafirishaji haramu wa binadamu; f) atataifisha, ataficha au ataharibu hati ya kusafiria au nyaraka za kusafiria za mtu anayesafirishwa kiharamu kwa lengo la kufanikisha usafirishaji haramu wa mtu huyo; g) anamzuia mtu anayesafirishwa kiharamu katika kupata msaada kutoka Jamhuri ya Muungano au kutafuta msaada kutoka serikali au mamlaka inayohusika; au h) kwa kujua anafaidika, kifedha au vinginevyo, au anatumia, nguvu au huduma ya mtu anayeshikiliwa chini ya masharti ya utumwa, ajira ya kulazimishwa au utumwa. (3) Mtu atakayefanya kosa chini ya kifungu hiki atawajibika, ikiwa akitiwa hatiani, kulipa faini isiyopungua shilingi milioni mbili na isiyozidi milioni hamsini au kufungwa kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka saba.
Usafirishaji haramu wa binadamu wa hali	**6**.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, baadhi ya vitendo au mazingira yataonekana kuwa ni usafirishaji

ya juu	haramu wa hali ya juu. (2) Usafirishaji haramu wa binadamu ulio juu utaoenekana ikiwa - a) mtu aliyesafirishwa ni mtoto au mtu mlemavu; b) kuasili kumefanyika kwa lengo la ukahaba, picha za ngono, unyonyaji wa kijinsia, ajira ya kulazimishwa na utumwa au dhamana ya deni; c) kosa limetendwa na mtandao wa watu au kwa kiasi kikubwa; d) mkosaji ni ndugu, mzazi, mtoto, mlezi au mtu mwenye mamlaka juu ya mtu anayesafirishwa kiharamu; e) kosa limefanyika na afisa wa umma, mfanyakazi au kiongozi wa dini; f) mtu aliyesafirishwa kiharamu anatumikishwa kwenye ukahaba na mjumbe yeyote wa jeshi au mamlaka ya utekelezaji wa sheria; g) mtendaji wa kosa ni mjumbe wa jeshi au mamlaka ya utekelezaji wa sheria; na h) kwa sababu au kwa kitendo cha usafirishaji haramu wa binadamu, mtu anayesafirishwa amekufa, amepata ugonjwa wa akili, ameathirika na Upungufu wa Kinga Mwilini (UKIMWI au AIDS), amepoteza kiungo chake, amepata magonjwa ya zinaa, magonjwa ya kuambukizwa au magonjwa mengine. (3) Kwaajili la kifungu kidogo (2)(c) usafirishaji haramu wa binadamu unaonekana kutendwa na mtandao wa watu kama- a) utafanyika na kundi la watu wawili au zaidi; au b) utafanyika dhidi ya watu watu wawili au zaidi, kwa peke yake au kama kundi. (4) Mtu atakayetenda kosa chini ya kifungu hiki atawajibika, kama akitiwa hatiani, kulipa faini isiyopungua shilingi milioni tano na isiyozidi shilingi milioni mia moja na hamisini au kufungwa kwa kipindi kisichopungua miaka kumi lakini kisichozidi miaka ishirini au vyote.
Usafirishaji haramu wa binadamu kwa kutumia watu wa	**7**.-(1) Mtu anayefanya kama mtu wa kati kwa lengo la usafirishaji haramu wa binadamu anafanya kosa.

kati.	(2) Kwa lengo la kifungu hiki - a) "mtu wa kati" maana yake ni mtu ambaye kwa kujua anashiriki au anahusika na kitendo chochote kile cha usafirishaji haramu wa binadamu chini ya Sheria hii; na b) " kuhusika " maana yake ni- i. kumpeleka au kumchukua mtu kwenye kitendo cha usafirishaji haramu wa binadamu; ii. kutoa ridhaa ili mtu asafirishwe kiharamu; iii. kumpokea mahali popote mtu kwa lengo la kumfanya mtu huyo asafirishwe kiharamu; au iv. kuingia makubaliano ya mdomo au maandishi kwa lengo la kumsafirisha mtu kiharamu au kusababisha mtu kuingia kwenye usafirishaji haramu wa binadamu. (3) Mtu atakayefanya kosa chini ya kifungu hiki atawajibika, akitiwa hatiani, kulipa faini isiyopungua shilingi milioni nne lakini isiyozidi shilingi milioni mia moja na hamsini au kufungwa kwa kipindi kisichopungua miaka saba lakini kisichozidi miaka kumi na tano au vyote
Kuwatumia watu waliosafirishwa kiharamu	**8.** Mtu anayenunua au anayetumia huduma ya watu waliosafirishwa kiharamu kwa ukahaba anatenda kosa na atawajibika, kama akitiwa hatiani, kulipa faini isiyopungua shilingi milioni moja lakini isiyozidi milioni thelathini au kufungwa kwa kipindi kisichopungua miezi kumi na mbili lakini kisichozidi miaka saba au vyote.
SEHEMU YA III UPELELEZI NA MWENENDO WA KIMAHAKAMA	
Usiri	**9.**-(1) Maisha binafsi na utambulisho wa mhanga wa usafirishaji haramu wa binadamu utatakiwa kuhifadhiwa na kulindwa. (2) Mamlaka za utekelezaji, majaji, watumishi wa

	mahakama na madaktari, pamoja na wahusika wakwenye kesi watawajibika, katika hatua yoyote ya uchunguzi au usikilizaji wa kesi chini ya Sheria hii, kutambua haki ya usiri ya mtu aliyesafirishwa kimakosa na mtuhumiwa. (3) Mahakama ambayo malalamiko yamepelekwa inaweza baada ya kuzingatia mazingira yote kwa maslahi ya pande zote, kuamuru mwenendo wa kesi kufanyika kwa siri. (4) Jina na taarifa binafsi za mtu aliyesafirishwa kiharamu au taarifa nyingine zinazohusiana na mtu aliyesafirishwa kiharamu hazitatakiwa kutolewa kwa umma. (5) Ikiwa uendeshaji wa mashitaka utafanyika kwa siri, itakuwa ni kinyume na sheria kwa- a. mhariri, mchapaji, mtangazaji au mwandishi; b. mtoa taarifa au mtayarishaji; c. mtayarishaji au mkurugenzi wa filamu, au d. mtu yeyote anayetumia vyombo vya habari au teknolojia ya mawasiliano, kusababisha kutangazwa kwa mwenendo huo wa mashitaka.
Kutoa taarifa ya makosa.	**10.** Mhanga wa usafirishaji haramu wa binadamu ambaye ana taarifa kuhusiana na mtu yeyote anayefanya vitendo vya usafirishaji haramu wa binadamu mahali pengine atatakiwa, kutoa taarifa ya kosa hilo kwa afisa wa polisi mara moja.
Kuhojiwa na afisa polisi	**11**.-(1) Kama afisa wa polisi akipokea taarifa kwa mujibu wa kifungu cha 10, afisa huyo atatakiwa- a) kumuhoji mtu anayetuhumiwa kutenda kosa la usafirishaji haramu wa binadamu; na b) kuweka kumbukumbu ya taarifa kwa undani. (2) Afisa wa polisi ambaye atakutana na mhanga wa usafirishaji haramu wa binadamu moja kwa moja atakuwa na wajibu wa jumla wa- a) kumsaidia mhanga kupata matibabu ya kitabibu na kisaikolojia, kama ni muhimu; b) kumsaidia mhanga kwa kumpeleka sehemu ya usalama kama mhanga ana mashaka na usalama; na c) kumwambia mhanga haki zake na msaada wa muhimu ambao utakuwepo ili kumsaidia mhanga.

Kukamatwa na afisa wa polisi	**12**.-(1) Afisa polisi haruhusiwi kumkamata mtu yeyote chini ya Sheria hii bila kibali cha kukamata (2) Bila kujali kifungu kidogo cha (1), afisa wa polisi anaweza kumkamata mtu kwa usafirishaji haramu wa binadamu bila kibali ikiwa- a) kitendo cha usafirishaji haramu wa binadamu kinafanyika wakati afisa huyo akiwepo; b) afisa wa polisi amezuiwa na mtuhumiwa kufanya upelelezi; c) mtu anataka kutenda kosa la usafirishaji haramu wa binadamu na hakuna njia ya kuzuia kutendeka kwa kosa hilo.
Kutenda kosa la pili na kuendelea	**13.** Mahakama inaweza kuongeza adhabu ambazo zimetajwa kwenye vifungu mbalimbali vya Sheria hii, kwa kutoa adhabu kali zaidi kwa mtu ambaye ametiwa hatiani kwa kosa la pili au zaidi kwenye Sheria hii.
Kutaifishwa kwa matunda na vifaa vilivyotokana na usafirishaji haramu wa binadamu	**14.**-(1) Kwa kuongezea kwenye adhabu inayotolewa kwa kutenda kosa chini ya Sheria hii, mahakama inaweza kuamuru kutaifishwa mapato yote na mali zilizotokana na kosa la usafirishaji haramu wa binadamu. (2) Fidia yoyote itakayotolewa itatakiwa kutoka kwenye mali binafsi na tofauti za mtuhumiwa isipokuwa kama mali hizo hazitatosha, ambapo salio litatakiwa kutoka kwenye mapato ya mali zilizotaifishwa. (3) Kama mapato, mali na vifaa vinavyohusiana na kosa la usafirishaji haramu wa binadamu vimeharibiwa, vimepoteza thamani au vinginevyo havifai kutoka na kutendo au kushindwa kutenda, moja kwa moja au si moja kwa moja, kwa mkosaji, au kimefichwa, kimeondolewa, kimebadilishwa au kimesafirishwa ili kuzuia kitu hicho kisipatikane au kuzuia kisitaifishwe, mtuhumiwa ataamuriwa kulipa kiasi sawasawa na thamani ya matunda, mali au kifaa kinachohusiana na kosa.
Fidia	**15**.-(1) Mtu atakayetiwa hatiani kwa kosa la usafirishaji haramu wa binadamu chini ya Sheria hii ataamuriwa na mahakama kulipa fidia kwa mhanga wa usafirishaji haramu wa binadamu. (2) Mtu atakayesababisha madhara kwa mtu yeyote katika usafirishaji haramu wa binadamu

	chini ya Sheria hii ataamuriwa kulipa fidia kwa mtu aliyedhurika. (3) Malipo ya fidia yatakuwani nyongeza ya adhabu yoyote iliyotolewa chini ya Sheria hii
Utambuzi wa wahanga	**16.** Utambuzi wa wahanga wa usafirishaji haramu wa binadamu utatakiwa kufanywa na afisa aliyeruhusiwa au mtu yoyote mwingine ambaye ana sababu za msingi za kuamini kuwa mtu ni mhanga wa usafirishaji haramu wa binadamu.
SEHEMU YA IV UOKOAJI, UBORESHAJI, ULINZI NA MSAADA KWA WAHANGA	
Kuwaokoa, kuwajali, kuwarejesha kwenye maisha ya kawaida na kuwashauri watu waliosafirishwa kiharamu	**17**.-(1) Afisa wa umma aliye kwenye ulinzi atawajibika kuwaokoa watu wanaosafirishwa kiharamu na kuwapa mahitaji ya msingi kwa ajili ya usalama na ulinzi, wahanga wa usafirishaji haramu wa binadamu waliookolewa. (2) Matibabu ya kijamii ya mhanga aliyeokolewa yatatakiwa kufanywa na maafisa wa ustawi wa jamii kwa lengo la kumrudisha mhanga kwenye hali yake ya kawaida na inaweza kujumuisha kumpatia msaada wakisheria na vifaa, kisaikolojia, kitabibu na kitaaluma, ajira na mahali pa kuishi. (3) Kamishna wa ustawi wa jamii atatakiwa kutoa ushauri nasaha kwa wahanga wa usafirishaji haramu wa binadamu kwa lengo la kuwasaidia ili warudi kwenye hali yao na ili waweze kujumuika na watu wengine. (4) Bila kujali masharti yaliyotajwa chini ya kifungu hiki, maslahi bora ya mtoto au mtu mlemavu yatatakiwa kutiliwa mkazo katika msaada wowote utakaotolewa wakati wa uokoaji, matibabu, ushauri nasaha na kumunganisha mtoto ambaye ni mhanga wa usafirishaji haramu wa binadamu.
Ulinzi na msaada kwa wahanga	**18.**-(1) Waziri kwa kushirikiana na Waziri anayehusika na ustawi wa jamii, atatakiwa kuchukua hatua stahili kwaajili ya ulinzi, matibabu na msaada kwa mhanga aliyeokolewa. (2) Ulinzi na msaada utakaotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) hautakuwa na sharti kuwa mhanga aliyeokolewa awe tayari kutoa maelezo na kushiriki kwenye uendeshaji wa mashitaka dhidi ya mtenda kosa la usafirishaji haramu wa binadamu.

	(3) Ulinzi, matibabu, msaada na huduma nyingine kwa mhanga aliyeokolewa utatolewa kulingana na uwepo wa rasilimali na unaweza kujumuisha - a) huduma ya bure ya kutafsiri kwa lugha watakayoichagua wenyewe; b) huduma ya bure ya mwanasheria kuhusiana na suala la usafirishaji haramu wa binadamu; c) huduma salama ya malazi ya muda, huduma ya kisaikolojia, kitabibu na kijamii kama itakavyoonekana muhimu kulingana na mahitaji; na d) huduma nyinginezo kama zitavyotolewa kwenye kwenye mwongozo wa kiutawala.
Msaada na Ulinzi kwa watoto wahanga.	**19.-**(1) Serikali itawajibika kutoa ulinzi, matibabu na msaada kwa mhanga wa usafirishaji haramu wa binadamu ambaye ni mtoto au mtu mwenye ulemavu huyo kuanzia pale itakapoaminika kuwa mtoto huyo au mtu mlemavu ni mhanga hadi pale ambapo uunganishwaji na jamii na atakapona kabisa. (2) Kama umri wa mhanga haujulikani lakini kuna sababu za kuamini kuwa mhanga hajatimiza umri wa miaka kumi na nane, itaaminika kuwa mhanga ni mtoto mpaka pale umri halisi utakapothibitishwa.
Vituo kwa ajili ya ulinzi wa wahanga	**20.**–(1) Serikali inaweza kwa ushauri wa Kikundi Kazi,kuanzisha au kutenga vituo kwa ajili ya ulinzi na msaada kwa wahanga wa usafirishaji haramu wa binadamu (2) Vituo vitakavyoanzishwa au kutengwa kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1) kitatakiwa kutoa malazi, chakula, msaada wa kisheria, huduma ya kisaikolojia na matibabu, usalama na ulinzi kwa wahanga wa usafirishaji haramu wa binadamu na pia kuwasaidia kuwatafuta ndugu zao.
Kuwarudisha makwao wahanga.	**21.**-(1) Serikali itahakikisha kuwa usafirishaji na upokeaji wa mhanga wa usafirishaji haramu wa binadamu ambao ni watanzania au wasiokuwa na taifa ambao wanastahili kupewa makao ndani ya Jamhuri ya Muungano baada ya kuingia kwenye eneo la nchi nyingine. (2) Serikali inaweza kuwezesha usafirishaji wa mhanga wa usafirishaji haramu wa binadamu ambaye hana nyaraka muhimu kwa kumpatia nyaraka za usafiri au kitambulisho chochote kitachotakiwa kwa ajili ya

	kumsafirisha
Kuwarudisha makwao wahanga watoto au watu wenye ulemavu	**22.** Mtoto au mtu mlemavu ambaye ni mhanga wa usafirishaji haramu wa binadamu atatakiwa kurudishwa nchini kwake ikiwa kabla ya kurudi kwake - a) mzazi, ndugu au mlezi wa kisheria ametoa ridhaa ya kumpokea mtoto au mtu mwenyeulemavu kuwa chini ya uangalizi wake; na b) wakala wa serikali au wakala wa ulinzi wa watoto kutoka nchi yake ametoa ridhaa na anaweza kuchukua wajibu wa kutoa msaada na ulinzi wa kutosha kwa mtoto.
Kuwarudisha makwao raia wa nje, nk..	**23**.-(1) Serikali itawajibika- a) kutoa msaada kwa raia wa nchi za nje na watu wasio na taifa ambao ni wahanga wa usafirishaji haramu wa binadamu mpaka watakaporudishwa kwenye nchi zao kwa ridhaa yao; na b) kuhakikisha usafirishaji wa wahanga wa usafirishaji haramu wa binadamu katika hali salama hadi kwenye mpaka wa Jamhuri ya Muungano (2) Bila kujali kifungu kidogo cha (1), mhanga wa usafirishaji haramu wa binadamu anaweza asirudishwe au asifukuzwe kwenda kwenye nchi yake ya asili au nchi ya tatu kama kuna sababu za msingi kuamini kuwa urudishwaji au ufukuzaji unaweza kumuweka mhanga kwenye hatari ya kupoteza uhai wake au kuhatarisha usalama wake au usalama wa familia yake. (3) Kama mhanga wa usafirishaji haramu wa binadamu hana nyaraka za kusafiria kutokana na kupotea, kuibiwa au kuharibiwa, Serikali itatakiwa, baada ya kuombwa na nchi ya nje, kusaidia katika upatikanaji wa nyaraka hizo kama itakavyokuwa muhimu ili kumwezesha mhanga kurudi kwenye nchi yake anakokaa
Programu zonazolenga usafirishaji haramu wa binadamu	**24.** Litakuwa ni jukumu la Serikali kuanzisha, kutekeleza na kuratibu program za kuzuia, kulinda na kuwatibu wahanga wa usafirishaji haramu wa binadamu. (a) kupitia Wizara inayohusika na mambo ya nje-

	i. kuweka tayari rasilimali na nyezo zilizo nje ya nchi kwa ajili ya watu waliosafirishwa kiharamu bila kujali njia walioyotumia kuingia kwenye nchi husika, na kutafuta njia ya kuboresha msaada wake katika kuondoa usafirishaji haramu wa binadamu kupitia mawasiliano ya karibu na wakala za serikali nchini na nje ya nchi, katika kuunda sera na utekelezaji wa program husika; ii. kuanzisha na kutekeleza program ya kabla ya ndoa, wakati wa ndoa na kabla ya kuondoka kwa ndoa zinazofungwa baina ya raia wanchi mbili; (b) kupitia wizara inayohusika na ustawi wa jamii- i. kutekeleza program za matibabu na ulinzi kwa watu waliosafirishwa kiharamu; ii. kutoa ushauri nasaha na makazi ya muda wa watu waliosafirishwa kiharamu na kuanzisha mfumo wa kutambua mashirika yasiyo ya kiserikali kwa lengo la kuanzisha vituo na programu za kukabiliana na usafirishaji haramu wa binadamu katika hatua mbali mbali kwenye jamii; (c) kupitia Wizara inayohusika na masuala ya kazi na ajira - i. kuhakikisha utekelezaji mahususi na ufuatwaji wa kanuni na miongozo inayohusiana na ajira kwa watu ndani na nje ya nchi; ii. kufuatilia, kuweka kumbukumbu na kutoa taarifa ya matukio wa usafirishaji haramu wa binadamu yanayowahusisha waajiri na watu wanaowatafutia waajiri wafanyakazi; (d) kupitia Wizara inayohusika na mambo ya sheria- i. kuhakikisha uendeshaji wa haraka wa mashtaka yanayohusiana na

	utendekaji wa makosa ya usafirishaji haramu wa binadamu; ii. kutenga na kuwafundisha waendesha mashtaka utaalamu maalumu katika kuendesha mashtaka ya makosa ya usafirishaji haramu wa binadamu; na iii. kuanzisha njia ya huduma za bure za kisheria kwa wahanga wa usafirishaji haramu wa binadamu.
SEHEMU YA V MFUKO WA KUZUIA USAFIRISHAJI HARAMU WA BINADAMU	
Uanzishwaji wa mfuko wa kuzuia usafirishaji haramu wa binadamu.	**25.** Unaanzishwa Mfuko wa Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu ambao kwenye Sheria hii utajulikana kama "Mfuko".
Vyanzo vya mfuko	**26.** Vyanzo vya fedha kwenye mfuko vitajumuisha- (a) kiasi cha fedha kama kitakavyotolewa na Bunge; (b) michango ya hiari kutoka kwa watu binafsi, mashirika yasiyo ya kiserikali na sekta binafsi zingine; (c) misaada na michango kutoka kwenye mashirika yenye mikataba; (d) kiasi chochote cha fedha au mali ambavyo mfuko unaweza kulipwa au kupewa; (e) kiasi chochote kingine cha fedha kinachoweza kuingizwa kwenye mfuko.
Matumizi ya mfuko	**27.** Mfuko utatumika kwa- (a) kusaidia mahitaji ya msingi ya wahanga wa usafirishaji haramu wa binadamu; (b) kutoa mafunzo wa wahanga wa

	usafirishaji haramu wa binadamu; (c) kutafuta familia za wahanga wa usafirishaji haramu wa binadamu; na kwa jambo lolote lile linalohusiana na matibabu na kuwarudisha wahanga wa usafirishaji haramu wa binadamu kwenye nchi zao kwa maslahi yao.
Usimamizi wa mfuko	**28.**-(1) Mfuko utasimamiwa na Sekretariati. (2) Fedha za Mfuko zitaingizwa kwenye akaunti ya Mfuko itakayofunguliwa kwa lengo hilo. (3) Vitabu vya akaunti vitatakiwa kukaguliwa kwa mujibu wa masharti yaliyoko kwenye Sheria ya Fedha za Umma.
Fedha, akaunti na makisio ya mwaka ya sekretariati.	**29**.-(1) Fedha za sekretariati zinajumuisha: (a) kiasi chochote cha fedha kitakachotengwa na Bunge kwa ajili ya sekratariati; (b) kiasi chochote kinachoweza kulipwa kwa sekretariati kwa njia ya mchango, zawadi au kupewa; na (c) kiasi chochote kinachoweza kudaiwa na Skretariati kwa njia ya ada ou malipo mengine kwa huduma iliyotolewa na Sekretariati. (2) Katibu atawajibika kutunza vitabu sahihi vya akaunti na kumbukumbu kuhusiana na mapato na matumizi ya mufuko kwa ajili ya Sekretariati. (3) Vitabu na akaunti za Sekretariati vitalazimika kukaguliwa kila mwaka na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. (4) Sekretariati itawajibika, si zaidi ya miezi mitatu kabla ya kuisha kwa kila mwaka wa fedha, kutayarisha na kuwasilisha kwa Waziri makisio ya kina ya mapato na matumizi kwa mwaka ujao wa fadha.
SEHEMU YA VI KAMATI YA KUZUIA USAFIRISHAJI HARAMU WA BINADAMU	
Uanzishwaji wa Kamati ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu.	**30.-**(1) Inaanzishwa Kamati ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu ambayo, kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 33 itawajibika kuainisha, kuchochea na kuratibu sera ya Serikali kuhusiana na kuzuia na kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu.

	(2) Kamati ya Kuzuia Usafirishaji haramu wa Binadamu itasaidiwa na Sekretariati ambayo itajumuisha watu wasiozidi nane watakaoteuliwa na Waziri. (3) Sekretariati itawajibika kuishauri Kamati ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu kuhusu masuala yanayohusiana na usimamizi wa jumla wa Sheria hii na masuala mengine yatakayoelekezwa kwa Waziri. (4) Sekretariati itaongozwa na Katibu ambaye atateuliwa na Rais kutoka Maafisa Waandamizi wa umma.
Muundo wa Kamati ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu.	**31**.-(1) Kamati ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu utaundwa na - a. mwenyekiti ambaye anateuliwa na Waziri kutoka kwa watu ambao wanashikilia au wamewahi kushikilia nafasi za Mkurugenzi wa Uhamiaji, Mkurugenzi Mkuu wa Polisi au Mkurugenzi wa Idara ya Intelenjisia na Usalama; b. mwakilishi kutoka Wizara inayohusika na Ustawi wa jamii ambaye hayuko chini ya cheo cha Mkurugenzi Msaidizi; c. mwakilishi wa Wizara inayohusika na wanawake na watoto ambaye hayuko chini ya cheo cha Mkurugenzi Msaidizi; d. mwanasheria kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye hayuko chini ya cheo cha Wakili wa Serikali Mwandamizi; e. mwakilishi kutoka Wizara ya Serikali ya Mitaa ambaye hayuko chini ya cheo cha Mkurugenzi Msaidizi; f. wato watano wakiwa ni wawakilishi kila mmoja kutoka Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Uhamiaji, Idara ya Usalama wa Taifa na Idara ya wakimbizi g. mwakilishi wa Wizara inayohusika na mambo ya nje; h. mwakilishi kutoka Idara ya Kazi ambaye hayuko chini ya cheo cha Kamishna Msaidizi wa Kazi; i. mwakilishi mmoja akiwakikisha sekta binafsi kama atavyopendekezwa na vyama visivyo vya

	Serikali; j. mwakilishi kutoka Wizara inayohusika na ustawi wa jamii kwenye Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar; k. mwakilishi kutoka Wizara inayohusika na wwnawake na watoto kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar; l. mwakilishi kutoka muungano wa vyama visivyo wa kiserikali vilivyoko Zanziba; m. mwakilishi kutoka Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; na n. wawakilishi wawili kutoka vvyama visivyo vya Serikali watakaoteuliwa na Waziri. (2) Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Kamati ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu watateuliwa na kuwajibika kwa Waziri.
Kazi ya Kamati ya Kuzuia Usafirishaji haramu wa Binadamu	**32.** Kamati ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu watafanya kazi zifuatazo- a. kuratibu shughuli za idara za serikali na vyombo vya utekelezaji wa sheria vvinavyojihusisha na mambo yanayohusiana na usafirishaji haramu wa binadamu; b. kutoa mapendekezo ya mpango ya taifa kwa ajili ya kikabiliana na usafirishaji haramu wa binadamu; c. kumshauri waziri kuhusu mambo ya sera yanayoendana na usafirishaji haramu wa binadamu; d. kutoa ushauri kuhusiana na upelelezi na uendeshaji mashtaka wa makosa yanayohusu usafirishaji haramu wa binadamu; e. kupendekeza na kuhimiza mbinu za kuzuia na kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu; f. kuwasiliana na wakala za Serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali katika kuwatibu na kuwarudisha kwenye jamii wahanga wa usafirishaji haramu wa binadamu; g. kuendana na viwango vya maendeleo ya kimataifa na kikanda katika kuzuia na kupambana na usafirishaji haramu wa

	binadamu ; na h. kutayarisha taratibu za utoaji wa fedha kutoka kwenye mfuko; na i. kushulikia suala lolote linalohusiana na usafirishaji haramu wa binadamu.
Vikao vya kamati ya Kuzuia usafirishaji haramu wa Binadamu	**33**.-(1) Kamati ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu inaweza kukutana katika muda ambao Mwenyekiti anaweza kuamua ikiwa italazimika kukutana angalau mara moja kila baada ya miezi mitatu. (2) Mwenyekiti ataongoza mikutano ya Kamati ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu ikiwa Mwenyekiti hatakuwepo, mjumbe wa Kamati ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu atakayechaguliwa na wajumbe watakaokuwepo ataongoza.
SEHEMU YA VII MASHARTI MADOGO	
Ulinzi wa kisheria kwa watu waliosafirishwa kiharamu.	**34.-**(1) Mhanga wa usafirishaji haramu wa binadamu hatatakiwa kushtakiwa au kuadhibiwa kwa makosa ambayo yanahusiana moja kwa moja na mashtaka ya makosa ambayo yametajwa kwenye Sheria hii. (2) Bila kujali masharti ya Sheria ya Uhamiaji, katika kumuondoa mhamiaji haramu, mhanga wa usafirishaji haramu wa binadamu aliye nchini kiharamu anaweza kubaki ndani ya Jamhuri ya Muungano katika kipindi chote cha upelelezi na uendeshaji wa mashtaka wa mkosaji na Serikali itaweka utaratibu wa kumrudisha mtu huyo kwao baada ya kukamilika kwa taratibu za kisheria. (3) Ikiwa ni kwa maslahi wa mhanga wa usafirishaji haramu wa binadamu anaweza kubaki ndani ya Jamuhuri ya Muungano baada ya taratibu za kisheria na kwa kibali cha Waziri anayehusika na mambo ya ndani. (4) Mtu anayeruhusiwa kubaki ndani ya Jamhuri ya Muungani kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (3) atakaa kwenye kituo cha mapokezi kitakachotolew na Serikali ambapo mtu huyo atapatiwa mahitaji yote

	ya msingi mpaka pale atakapopata makazi ndani ya Jamhuri ya Muungano. (5) Baada ya kumtia hatiani mtu anayetuhumiwa kwa kosa la usafirishaji haramu wa binadamu, mhanga wa usafirishaji haramu wa binadamu atakaa kwenye kituo cha Serikali ambapo mtu huyo atapatiwa mahitaji yote ya msingi mpaka pale atakapopata makazi ndani ya Jamhuri ya Muungano.
Ulinzi kwa wajumbe	**35.** Hakuna kitendo au kitu au kutofanya kitu kutakakofanywa na mjume wa Kamati ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu au Sekretariati, kama kumefanywa au kumeshindwa kufanyika, kwa nia njema katika utekelezaji wa kazi au katika kutumia mamlaka chini ya Sheria hii, kutawafanya kuwajibika wao wenyewe kwa kutenda au kushindwa.
Matumizi ya sheria nyingine. Sura ya 214 Sura ya 20	**36**.-(1) Mtu ambaye si raia za Tanzania ambaye anafanya kosa la usafirishaji haramu wa binadamu atawajibika kwenye mwenendo wa kusafirishwa chini ya Sheria ya Kubalishana. **(2)** Masharti ya Sheria hii kama ambavyo yatahusiana na mamlaka ya afisa wa polisi, yatakuwa ni nyongeza ya mamlaka yaliyotolewa chini ya Sheria ya Polisi na sheria zinazohusiana na mwenendo wa makosa ya jinai isipokuwa kwamba, kama kuna mgongano, Sheria hii itatumika.
Kanuni	**37.** Waziri anaweza kwa kushauriwa na Kamati ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, kutengeneza kanuni zikieleza- (a) hatua za kuzuia zinazotakiwa kuchukuliwa na vyombo mbalimbali vya serikali dhidi ya usafirishaji haramu wa binadamu kwa kazi za kinyonyaji; (b) mafunzo ya kupambana na na usafirishwaji haramu wa binadamu kwa wafanyakazi wa vyombo vya usalama; (c) kukusanya takwimu na kubadilishana taarifa zinazohusiana na usafirishaji haramu wa binadamu; (d) matibabu na kuwarudisha kwenye jamii wahanga wa usafirishaji haramu wa binadamu; (e) utaratibu wa kuwalinda, kuwatibu na msaada katika kuwashughulikia watoto ambao ni wahanga wa usafirishaji haramu wa

	binadamu; na (f) jambo lolote ili kufanikisha utekelezaji mzuri wa Sheria hii
SEHEMU YA VIII MAREKEBISHO YA SHERIA YATOKANAYO	
Kufutwa kwa kifungu cha 139A, Sura ya 16	**38**. Sheria ya Kanuni ya Adhabu inarekebishwa kwa kufutwa kifungu cha 139A.
Kurekebishwa kwa kifungu cha 148, Sura ya 20	**39.** Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai inarekebishwa katika kifungu cha 148(5) kwa kutoa nukta iliyopo kwenye aya ndogo ya (v) ya aya ya (a) na badala yake kuweka koloni ndogo na baada ya hapo kuongeza yafuatayo- "(vi) usafirishaji haramu wa binadamu chini ya Sheria ya Kuzuia Usafirishaji haramu wa Binadamu."
Kurekebishwa kwa kifungu cha 10, Sura ya 54	**40.** Sheria ya Uhamiaji inarekebishwa katika kifungu cha 10(1) kwa kuondoa nukta iliyopo katika aya ya (k) na badala yake kuweka koloni ndogo na baada ya hapo kuongeza aya ifuatayo- "(l) mtu aliyefanya kosa la usafirishaji haramu wa binadamu."
Kurekebishwa kwa kifungu cha 3, Sura ya 423	**41.** Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Fedha inarekebishwa katika kifungu cha (3) kwa kuondoa aya ya (e) inayoonekana katika maana ya "predicate offence" na badala yake kuweka aya ifuatayo- "(e) usafirishaji haramu wa binadamu na kuvusha wahamiaji haramu kinyume na sheria.

Imepitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania terehe 11 April, 2008